



Piga simu kwa mtaalamu wa rufaa ya mzazi wa CCR&R kwa
usaidizi wa kufahamu utunzaji wa watoto katika Iowa.


855-244-5301



Child Care Search ni zana ya kutafuta mtandaoni inayokusaidia kupata utunzaji wa watoto karibu na nyumbani, kazini au vituoni kwenye njia yako. Ili kuanza, weka tu anwani yako ya nyumbani kama mahali pa kuanzia na unakoenda, kisha uone matokeo.

<https://childcaresearch.iowa.gov>

Aina ya utunzaji



Kituo/Shule ya Mapema

- Kupewa leseni na Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya Iowa (HHS) kila baada ya miaka miwili
- Ukaguzi mmoja wa kila mwaka kutoka kwa wafanyikazi wa kutoa leseni wa HHS
- Wafanyakazi wote ambao wana mawasiliano na watoto wamekuwa na ukaguzi wa rekodi ya Usajili wa Unyanyasaji wa Iowa na ukaguzi wa historia ya uhalifu
- Wafanyakazi wote zaidi ya 18 wamechukuliwa alama za vidole
- Wafanyakazi wote wanatakiwa kupewa mafunzo ya Urejeshaji Wa Kupumua Na Mapiyo Ya Moyo (CPR) na Huduma ya Kwanza, Ripota wa Lazima wa Unyanyasaji wa Watoto, Utunzaji Muhimu wa Malezi ya Watoto na Tahadhari za Kiulimwengu.
- Wafanyakazi wote wanahitaji saa 6 za kuendelea na masomo kila mwaka

Makazi ya Malezi ya Watoto A, B, C1, na C

- Kusajiliwa na HHS kila baada ya miaka miwili (anaweza kuitwa mtoa huduma aliyesajiliwa)
- Ukaguzi wa kila mwaka kutoka kwa HHS
- Mtu yeyote mwenye umri wa miaka 14 au zaidi anayeishi nyumbani ana ukaguzi wa rekodi ya Usajili wa Unyanyasaji wa Iowa na ukaguzi wa historia ya uhalifu
- Mtoa huduma na mtu yeyote mwenye umri wa miaka 18 au zaidi anayeishi nyumbani wamechukuliwa alama za vidole
- Watoa huduma wanahitaji saa 24 za elimu inayoendelea katika kipindi cha miaka 2 ya usajili.

Nyumba ya Kulelea Watoto imeidhinishwa kwa Usaidizi wa Malezi ya Mtoto (CCA)

- Kuwa na Makubaliano ya Mtoa Huduma ya Usaidizi wa Watoto na HHS
- Ukaguzi wa kila mwaka kutoka kwa HHS
- Mtu yeyote mwenye umri wa miaka 14 au zaidi anayeishi nyumbani ana ukaguzi wa rekodi ya Usajili wa Unyanyasaji wa Iowa na ukaguzi wa historia ya uhalifu
- Watoa huduma wanahitaji saa sita za kuendelea na elimu katika kila makubaliano ya miaka miwili

Nyumba ya Malezi ya Watoto:

- Hadhibitiwi na Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya Iowa (HHS) (anaweza kuitwa mtoa huduma ambaye hajasajiliwa)
- Haina Makubaliano ya Mtoa Huduma ya Usaidizi wa Mtoto (CCA) na HHS

KUMBUKA: Mafunzo yanayohitajika kwa watoa huduma wote waliosajiliwa: CPR/Huduma ya Kwanza, Ripota wa Lazima wa Unyanyasaji wa Watoto & Huduma Muhimu ya Malezi ya Watoto